COMPETENCE BASED CURRICULUM HOMEWORK ENGAGEMENT PROGRAM GRADE 2 2024 AUGUST KISWAHILI 1

1. **SEHEMU YA A: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA**

    1. Shuleni ni mahali pa kufanyia nini?
    2. Uwanja wa shuleni hutumiwa kufanyia nini.
    3. Je, mlinzi hufanya kazi gani shuleni?
    4. Wewe huweka vitabu vyako wapi?
    5. Wanafunzi wakiwa shuleni huenda haja ndogo au kubwa wapi?

2. **SEHEMU YA B: KUSOMA KWA SAUTI.**

    Soma hadithi hii kwa sauti.

    Mwalimu alikuwa ametuambia kuwa mvua inapoanza kunyesha tukicheza,

    twende tukajikinge ili tusinyeshewe. Siku hiyo tulikuwa

    tukicheza mpira. Mara, mvua ikaanza kunyesha. Tulichukua mpira wetu na kuelekea darasani mbio. (Alama 5)

3. **ZOEZI LA 3: KUSOMA KWA UFAHAMU** Soma

    hadithi hii na ujibu maswali yafuatayo.

    Tuliondoka shuleni wakati wa asubuhi kuelekea katika mtaa wa Poromoka. Tulifaa kwenda kupanda miti kwa sababu watu wa Poromoka walikuwa wamekata miti ili kuchoma makaa. Mwalimu alitubebea miche nasi tukabeba majembe. Tulitakiwa kumaliza kazi saa nane.

    11. Wanafunzi walitoka shuleni wakati wa _____.
    12. Mtaa uliotajwa unaitwa mtaa wa _____.
    13. Watu walikuwa wamekata miti ili kuchoma _____.
    14. Ni nani aliyebeba miche?
    15. Wanafunzi hawa walibeba _____.

4. **ZOEZI LA 4: SARUFI**

    Andika sentensi hizi katika hali ya wingi.